



ST. FRANCIS UNIVERSITY COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES (SFUCHAS)



A Constituent College of St. Augustine University of Tanzania

P.O. Box 175
Ifakara, Tanzania

Phone: (255) 23-2931-568
Fax: (255) 23-2931-569

Email: principal@sfuchas.ac.tz
Website: www.sfuchas.ac.tz

10/10/2023

TANGAZO LA ZABUNI YA HUDUMA YA ULINZI

Chuo Kikuu Kishiriki Cha Tiba na Afya Cha Mtakatifu Fransisko Ifakara, kinakaribisha maombi ya uzabuni wa huduma ya Ulinzi kwa wanachuo, wafanyakazi, mali za Chuo na wageni wa Chuo, kutoka kampuni au taasisi yoyote ya ulinzi iliyo sajiriwa kisheria.

Chuo chetu kinapatikana ndani ya Mkoa wa Morogoro katika Wilaya ya Kilombero Mjini Ifakara. Chuo kipo umbali wa km 426 kutoka Dar es Salaam. Unaweza kutumia usafiri wa bus au train kutoka Dar es Salaam kuja Ifakara.

MWOMBAJI ANATAKIWA KUWA NA VIGEZO VIFUATAVYO

A. VIGEZO VYA JUMLA KWA MWOMBAJI

- Awe tayari kufanya kazi katika eneo ambalo Chuo kitampangia kwa matumizi ya huduma husika.
- Awe tayari kuthibitisha uwezo alionao kifedha kuendesha shughuli anayoomba kwa kuleta taarifa zake za kibenki (Bank Statement) za miezi mitatu ya mwisho
- Awe na leseni halali ya biashara ya huduma husika
- Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu wa kutoa huduma katika zabuni anayoomba
- Mwombaji itabidi alipe ada ya maombi ya Tshs 100,000/= (Laki moja tu). Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya CRDB Bank Jina St. Francis University College Akaunti namba **0150261537600** na kuambatanisha risiti ya malipo.

B. VIGEZO VYA NYONGEZA

- ✓ Awe na kampuni ya ulinzi iliyosajiliwa rasmi
- ✓ Awe na walinzi waliofuzu mafunzo stahiki ya ulinzi (Paramilitary)
- ✓ Awe na walinzi waliohakikiwa kuwa hawajahusika katika makosa ya jinai

(Vetted by Police to be crime free)

- ✓ Awe na zana za kisasa za ulinzi za kumuwezesha kukabiliana na changamoto za kiusalama (Security Devices, Security alarm system, transportation).

Utaratibu wa kurejesha nyaraka za uzabuni utakuwa kama ifuatavyo

Mwombaji atatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Nakala ya leseni ya biashara
 - Nakala ya namba ya mlipa kodi (TIN Number)
 - Nakala ya usajili (Certificate of Registration)
 - Taarifa za Benki (Bank Statement)
 - Anuani ya makazi
 - Namba ya Simu
 - Mahali Ofisi inapopatikana (Mkoa, Wilaya, Kata, Mtaa)
- ✓ Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe **9/ 11/2023 saa 4:00 asubuhi**.
Maombi yatakayofika baada ya muda huo hayatapokelewa
 - ✓ Maombi ya zabuni yatafunguliwa **tarehe 14/11/2023 saa 5:00 asubuhi** katika ukumbi wa mikutano, mbele ya waombaji wote
 - ✓ Chuo kitamtaarifu mzabuni aliyeshinda kwa maandishi.

Maombi yote yatunwe kwa njia ya Barua Pepe *principal@sfuchas.ac.tz* au kwa anuani ya posta *S.L.P 175, Ifakara*.


Kwa Maelezo zaidi wasiliana na Chuo Kikuu Cha Mtakatifu Fransisko IFAKARA

Simu +255 23 2931 568/0784 514 246

Ndimi,



Prof. Fr. Juvenalis Baitu



Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Utawala na Fedha